# Nafasi ya Nyimbo za Kizazi Kipya katika Kufundishia Masuala Mtambuko katika Mtaala wa Umilisi

*Nyandwaro K. Lena* na *Alfred Malugu*
*Chuo Kikuu cha Rongo*

**Ikisiri**

**Hitaji mojawapo katika Mtaala wa Umilisi nchini Kenya ni kuwa wanafunzi wanapaswa kufundishwa masuala mtambuko. Lengo la kuwafundisha masuala mtambuko ni kuwasaidia wawe wabunifu na wapate ujuzi wa kukabiliana na masuala haya katika mazingira yao ya kila siku. Mtaala huu unasisitiza kuwa mwalimu anapaswa kuwa mbunifu katika ufundishaji wake ili kukuza umilisi wa wanafunzi. Njia mojawapo ya kufundisha masuala kiubunifu ni kupitia matumizi ya nyimbo za kizazi kipya ambazo zina maudhui ya masuala mtambuko mbalimbali. Nyimbo hizi zinapendwa na vijana ambao hujihusisha nazo na wao huzisikiliza kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Makala haya yanachanganua baadhi ya nyimbo za kizazi kipya na jinsi mwalimu anavyoweza kuzitumia kufundishia masuala mtambuko darasani ili kufikia malengo yake na matarajio ya jamii kwa ujumla. Nadharia iliyoongoza makala haya ni Nadharia ya Utekelezaji wa Mtaala iliyoasisiwa na Gross (1971).**

**Maneno Muhimu:** *Mtaala wa Umilisi, Masuala Mtambuko, Nyimbo za Kizazi Kipya*

**Utangulizi**

Kulingana na IBE-UNESCO (2017), mtaala hutumiwa kuwapa wananchi wake maarifa, ujuzi, thamani na mielekeo faafu ili wafikie malengo yao ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Utafiti uliofanywa na Tume ya Kukuza Mtaala Nchini Kenya (2017) ulibaini kuwa Wakenya walipendelea kuwapo na mtaala ambao ungewasaidia wanafunzi kutumia maarifa waliyopata shuleni kukabiliana na maisha yao ya kila siku. Hali hii ilichangia kuwapo na mabadiliko katika mtaala wa elimu nchini Kenya kutoka matumizi ya Mtaala wa 8-4-4 ambao ulikuwa umetumika zaidi ya miongo mitatu hadi Mtaala wa Umilisi. Abuya (2017) anaeleza kuwa Mtaala wa Umilisi umeweka mahitaji ya mtoto mbele ya yale ya shule, mwalimu na wazazi. Lengo la mtaala huu ni kuhakikisha kuwa maarifa ambayo mwanafunzi amepata shuleni anayatumia kutekeleza shughuli mbalimbali katika mazingira yake halisi anamokulia kila siku (Sifuna na Obonyo, 2019).

Katika Mtaala wa Umilisi, kuna ufundishaji wa masuala mtambuko. Masuala haya yameainishwa katika vitengo sita: stadi za maisha, uraia, utangamano, umoja wa kijamii, kujiamini na elimu kwa maendeleo endelevu. TUKI (2013) wanaeleza kuwa masuala mtambuko ni mambo, mada au shughuli zinazovuka na kuhusisha sehemu zingine katika jamii. Ni masuala ambayo yapo nasi na yanaathiri kila mwanajamii awe mtoto au mtu mzima kwa njia moja au nyingine. Masuala haya hutokea kama matatizo ambayo yanahitaji suluhisho katika jamii. Hivyo basi, Tume ya Kukuza Mtaala Nchini Kenya (2017) inapendekeza kuwa ni muhimu wanafunzi wafundishwe masuala haya na jinsi ya kukabiliana nayo. Pendekezo hili lilitokana na ripoti kuhusu ufundishaji wa stadi za maisha (2012), ripoti kuhusu wajibu wa mtaala katika kuleta uwiano wa kitaifa (2013), ripoti ya uhakiki wa kutekeleza ufundishaji wa masuala ibuka (2014) na ripoti ya uhakiki wa yaliyomo yanayohusiana na masuala ibuka (2016). Ripoti hizi zilibaini kuwa ni muhimu wanafunzi kufundishwa masuala mtambuko kwani ulimwengu unabadilika kila uchao na pana haja ya wao kuwa na maarifa ya kukabiliana na masuala haya moja kwa moja na kwa njia inayofaa.

Ufundishaji wa masuala mtambuko ni muhimu kwani kwa mujibu wa Sultana na Naseem (2012), husaidia wanafunzi na walimu kuelewa kwa kina ubora, changamoto, ubunifu na mabadiliko yanayotokea kitaifa na kimataifa. Ingawa imebainika kuwa ni muhimu wanafunzi kufundishwa masuala haya, tafiti zimeonyesha kuwa ufundishaji wake haujatekelezwa kikamilifu na kwa njia inayofaa (Ondimu 2018, Sifuna na Obonyo 2019 na Owala 2021). Gitau na wenzake (2023) walibaini

kuwa walimu hawakuwa na maarifa ya kutosha ya kufundisha masuala mtambuko. Pia, walipofundisha masuala haya, walitumia mbinu za kimapokeo za mihadhara na majibu na maswali. Mbinu hizi ziliashiria mwalimu kukosa ubunifu wa kufundisha masuala mtambuko. Omollo na wenzake (2016) wanaeleza kuwa ni muhimu mwalimu kubuni mbinu bunifu anapofundisha wanafunzi wake ili somo analofundisha liwe la kufana na wanafunzi wafurahie. Hivyo basi, ni muhimu mwalimu kuteua mbinu za ufundishaji zilizo bunifu na zitakazomsaidia mwanafunzi kutagusana na mazingira yake ili afikie kilele cha utendaji katika mazingira halisi, jambo linalosisitizwa katika Mtaala wa Umilisi (Khalili, 2018 na Gitau na wenzake, 2023). Njia mojawapo ya ubunifu ambayo mwalimu anaweza kutumia kufundisha masuala mtambuko ni kupitia nyimbo za kizazi kipya. Wasike (2015) anaeleza kuwa mwalimu bunifu anaweza kutumia nyimbo anapofundisha masuala mtambuko. Hii ni kwa sababu nyimbo husisimua wanafunzi na hivyo kuimarisha kumbukizi yao kuhusu waliyofundishwa.

**Dhana ya Nyimbo za Kizazi Kipya**

Mulokozi (2017) anaeleza kuwa, kadri dunia inavyobadilika ndivyo fasihi simulizi inavyobadilika ili kukidhi malengo na matakwa ya jamii. Hali hii imezua vipera vipya katika tanzu za fasihi simulizi kama vile nyimbo za kizazi kipya ambazo hutungwa na kuimbwa na vijana kutoka jamii mbalimbali. Kulingana na Ntarangwi (2009) na Mwangi (2004), nyimbo za kizazi kipya ni zao la utandawazi na mabadiliko ya mifumo mbalimbali katika jamii. Nyimbo hizi zilizuka miaka ya 1980 ili kukidhi mahitaji ya wanajamii hasa ya vijana na kusambaa kupitia vyombo vya habari.

Kebaya na Wanjala (2016) wanaeleza kuwa nyimbo za kizazi kipya zina mguso na athari ya juu miongoni mwa vijana nchini Kenya kwa sababu zinawatambulisha katika jamii wanamoishi. Pia, ni nyimbo zinazowahamasisha vijana ambao mara nyingi huwa wamepuuzwa katika jamii. Isitoshe, huwatambulisha vijana wa Afrika Mashariki kwa dunia. Zaidi ya hayo, huwa ni jukwaa la kuhakiki masuala ya kitaifa na kimataifa katika ngazi zote za jamii, na huelezea hisia za kweli kuhusu matarajio ya vijana katika jamii zao. Koster (2013) anakiri kuwa nyimbo hizi zimeleta mapinduzi miongoni mwa vijana wanaoishi mijini na kupitia vyombo vya habari, kuwafikia vijana walio vijijini. Anaeleza kuwa ujumbe unaopatikana katika nyimbo hizi huzindua na kuuwauganisha vijana kutoka makabila na matabaka yote, huponya mioyo yao na kupanda mbegu za mabadiliko miongoni mwao. Kwa upande mwingine, Purello (2011) anasema kuwa maudhui yanayopatikana katika nyimbo hizi, huibua hisia kali na majibu kwa matatizo na changamoto zinazowakumba vijana. Anazidi kusema kuwa nyimbo hizi husaidia katika kuleta mabadiliko katika jamii hasa palipo na mikwaruzano miongoni mwa wanajamii. Pia, huleta utambuzi wa masuala mbalimbali miongoni mwa vijana na wanajamii wote. Naye Njogu (2009) anafafanua kuwa nyimbo za kizazi kipya huchochea mawazo yenye jumbe nzito na huwasilishwa kupitia mbinu za lugha za kiwango cha juu.

Ni wazi kuwa nyimbo za kizazi kipya hutungwa kwa ubunifu wa juu na kupitia maudhui yake, mwalimu anaweza kutumia kufundisha masuala mtambuko. Hii ni kwa sababu wanafunzi wengi hufahamu nyimbo, hivyo basi wanaweza kuchangia na kuibua mijadala darasani, hali ambayo inasisitizwa katika Mtaala wa Umilisi yaani kuhusishwa kwa wanafunzi katika ufundishaji. Pia, kwa kutumia nyimbo za kizazi kipya katika kufundisha masuala ibuka, matumizi ya teknolojia itahusishwa pale ambapo nyimbo zitatafutwa katika mitandao ya kijamii kama You Tube, Spotify, mdundo na boomplay jambo linalosisitizwa katika Mtaala wa Umilisi yaani matumizi ya teknolojia katika ufundishaji.

Ni muhimu kutaja kuwa waimbaji wa nyimbo hizi huchanganya lugha katika uimbaji wao. Wao hutumia Kiswahili, Kiingereza, lugha za kiasili na sheng' katika kupitisha ujumbe kwa wanajamii. Hali hii hufanya nyimbo hizi kuwafikia wanajamii wengi, wakubwa kwa wadogo, vijana kwa wazee.

**Nadharia ya Utafiti**

Nadharia iliyoongoza makala haya ni Nadharia ya Utekelezaji wa Mtaala iliyoasisiwa na Gross (1971). Nadharia hii inaeleza kuwa ili utekelezaji wa mtaala wowote uwe faafu, ni sharti ifuate yafuatayo ambayo pia ni mihimili ya nadharia hii. Kwanza, ni kuwa mtekelezaji wa mtaala ambaye ni mwalimu anatarajiwa kuelewa mtaala husika. Pili, mwalimu anapaswa kuwa na umilisi wa kutosha wa kutekeleza mtaala husika. Tatu, kuwapo na mbinu na njia zinazofaa za kutekeleza mtaala husika

na mwisho, mwalimu apewe msaada wa kutosha kutoka kwa wadau mbalimbali katika sekta ya elimu. Katika makala haya, mhimili wa mwalimu kufahamu mtaala husika na kutumia mbinu ya nyimbo za kizazi kipya kutekeleza ufundishaji wa masuala mtambuko ulizingatiwa.

**Uhakiki wa Masuala Mtambuko Kupitia Nyimbo za Kizazi Kipya**

Masuala mtambuko yaliyoshughulikiwa katika makala haya ni dawa za kulevya, magonjwa, uhifadhi wa mazingira, ugaidi, vita vya kikabila baada ya uchaguzi, ufisadi, uzalendo, ajira na bidi, na suala la athari za ngono ya mapema miongoni mwa vijana. Masuala haya yamechanganuliwa kwa kuzingatia nyimbo teule za kizazi kipya zilizo na maudhui ya masuala haya. Mwalimu anapotayarisha vipindi vyake, anaweza kutafuta nyimbo hizi, kisha akazicheza darasani kupitia vyombo vya habari na kuwaelekeza wanafunzi katika kuzichambua na kuhakiki namna zinavyoeleza masuala mtambuko.

**Suala la Dawa za Kulevya**

Suala la dawa za kulevya limekuwa ni kero katika jamii kutokana na athari zake hasi. Kulingana na ripoti ya NACADA (2016), mazingira ya shule za upili ni eneo mojawapo ambalo vijana hutumia dawa za kulevya. Ripoti hiyo inaeleza kuwa matumizi ya dawa za kulevya huanzia umri wa miaka 13 hadi 15. Kinachosikitisha ni kuwa hakuna usimamizi na maelekezo makali kuhusu ukomeshaji wa matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana nyumbani na mashuleni. Kwa hivyo, ripoti hii inapendekeza kuwe na mafundisho kuhusu dawa za kulevya, athari zake na namna ya kuepuka matumizi yake katika mtaala wa elimu nchini Kenya. Kutokana na pendekezo hilo, dawa za kulevya ni suala mtambuko ambalo limeorodheshwa chini ya kitengo cha elimu ya afya (K.I.C.D 2017) kwenye Mtaala wa Umilisi.

Katika suala hili, mwalimu anaweza kutumia nyimbo za kizazi kipya zilizo na maudhui kuhusu dawa za kulevya kuelimisha wanafunzi. Kwa mfano, kupitia wimbo wa *Drug si Swagg* ulioimbwa na Kibet wakishirikiana na Mike. 'Swagg' ni neno la Kiingereza ambalo katika lugha ya Sheng' humaananisha mtu mtulivu au anayependeza kupitia yale anayoyafanya kwa jamii. Kwa hivyo, kupitia mada ya wimbo huu mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi waeleze maoni yao kuhusu matumizi ya dawa za kulevya; yaani ikiwa ni jambo nzuri au mbaya.

Kupitia maudhui yake, mwalimu na wanafunzi wanaweza kuchambua aina za dawa za kulevya na madhara ya dawa hizo kama zinavyojitokeza katika wimbo huo. Waimbaji wa wimbo huu wanaorodhesha dawa za kulevya kama vile pombe, sigara, bangi, mirungi (miraa) na heroini. Wanaimba kuwa *When you are drug free, you are free but when you are on drugs, you stagger Drug causes hallucinations among the youth* kumaanisha kuwa wakati vijana hawatumii dawa za kulevya wako huru ila wanapotumia, hawawezi kuwa wima akilini na kiafya kwani dawa za kulevya husababisha njozi zisizo za kweli. Hii ni athari hasi mojawapo ya dawa za kulevya.

Mwimbaji wa wimbo huu katika mahojiano yake na wanahabari, anaeleza kuwa alianza kutumia dawa za kulevya akiwa shule ya upili, na anaeleza namna zilivyomwathiri kiafya, masomo yake na safari yake ya kuacha kutumia dawa hizo. Mwalimu anaweza kutumia mahojiano yake kama mfano kwa wanafunzi ambao wanatumia dawa za kulevya kuwa mtu anaweza kuacha kutumia dawa za kulevya na kuishi maisha yenye afya.

Kupitia wimbo wa Stivo Simple Boy *Vijana Tuwache Mihadarati*, anaeleza madhara mengine ya dawa za kulevya huku akiwarai vijana waache kabisa matumizi ya dawa za kulevya. Anaeleza kuwa *mihadarati huharibu akili, mwili na vijana hushindwa kufanya kazi. Husababisha vifo miongoni mwa vijana, saratani na hufanya vijana kufanya mapenzi kiholela*, hali ambayo inaweza kuchangia maambukizi ya magonjwa ya zinaa pamoja na virusi vya UKIMWI. Isitoshe, anaeleza kuwa matumizi ya dawa za kulevya huchangia utamaushi miongoni mwa wazazi wa vijana wanaotumia dawa za kulevya. Wimbo huu unaweza kutumiwa na mwalimu kufundisha na kutahadharisha wanafunzi dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya. Hali hii itachangia katika kukabiliana na suala hili ili kuwapo na jamii ambayo vijana wake hawatumii dawa za kulevya na hivyo kuwa na kizazi chenye vijana wenye afya njema.

**Suala la Magonjwa**

Magonjwa yanayoshughulikiwa katika makala haya ni UKIMWI, saratani na afya ya akili.

**Ugonjwa wa UKIMWI**

Hili ni suala mtambuko ambalo linapaswa kufundishwa katika Mtaala wa Umilisi. Ni ugonjwa ambao umekuwapo zaidi ya miongo mitatu na huathiri kila mwanajamii moja kwa moja au kupitia wanajamii wenzake. Ripoti ya National Aids Control Council (2018) inaeleza kuwa asilimia 9 ya vijana waliobalehe kati ya miaka 10-19 wanaishi na VVU na asilimia 48 huambukizwa virusi hivi kila siku. Vijana 8 hufa kila siku kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Mwaka wa 2017, asilimia 40 ya maambukizi mapya ya VVU miongoni mwa wanajamii walikuwa kati ya umri wa 15 hadi 24. Ripoti hii inaashiria kuwa pana haja ya wanafunzi kufundishwa suala la VVU/UKIMWI kwani maambukizi katika kiwango cha juu huwa miongoni mwao.

Kumekuwa na mafundisho kuhusu namna ya kujikinga kutokana na VVU na namna ya kuishi na virusi hivi ikiwa mtu ameambukizwa. Pia, pana msisitizo kutoka kwa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) kwamba vijana wachukue hatua ya kuanza kujipima virusi hivi katika mazingira ambayo hawatakuwa na uoga nayo. Hali hii ilitokana na utafiti uliofanywa na shirika hilo mwaka wa 2015 ambapo walibaini kuwa changamoto mojawapo inayozuia hatua chanya kupigwa katika kupambana na ugonjwa huu ni uoga na unyanyapaa miongoni mwa vijana kwenda vituo vya kupima virusi hivi (V.C.T) au hospitalini.

Kwa hivyo, mwalimu anaweza kufundisha suala hili la vijana kuchukua hatua ya kujipima VVU nyumbani ama popote pale kwa kutumia vipimo halisi vinavyopatikana kwenye maduka ya kuuza dawa kupitia wimbo wa *Chukua Selfie* ulioimbwa na kundi la wanamuziki kutoka nchini Kenya. Maana ya juu ya kirai *Chukua Selfie* ni kujipiga picha kwa kutumia rununu lakini katika maana ya ndani ni kujua hali yako kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kwa kujipima. Wimbo huu unasisitiza jukumu la vijana kujua hali yao kabla ya kushiriki ngono. Mwalimu anaweza kutumia beti zifuatazo za wimbo huu kuwafundisha wanafunzi wake: Ubeti unaoimbwa na msanii Jua Cali…*jiamini chukua selfie* kwa maana kuwa kijana anayehusika asiwe na uoga wa kujua hali yake. Ubeti unaoimbwa na Fena Gitu…*before we get down to business, piga selfie, mimi na ma lover chukua selfie* kwa maana kuwa kabla ya kushiriki ngono, wanaohusika ni muhimu wajipime ili kujua hali yao ya UKIMWI. Ubeti wa Naiboi…*we all know you know yourself…chukua selfie* kwa maana kuwa sote tunajua unajua hali yako ya VVU/UKIMWI, hata hivyo ni muhimu kujipima. Kutokana na beti hizi, wanafunzi watafundishwa umuhimu wa kuwa wajasiri wa kujua hali zao kuhusu VVU/UKIMWI na hivyo kuishi bila uoga, kuchukua tahadhari na hivyo kusaidia katika kupunguza uenezaji na msambao wa ugonjwa huu.

**Ugonjwa wa Saratani**

Ugonjwa wa saratani umewaathiri wanajamii sana kiafya na kiuchumi kutokana na ughali wake kimatibabu. Ni ugonjwa ambao upo nasi na pana haja ya kuwafundisha wanafunzi kuihusu. Busolo na Decker (2018) wanaeleza kuwa idadi ya watu wanaougua ugonjwa wa saratani unaongezeka duniani kila uchao. Wanaeleza kuwa pana uwezekano mkubwa siku za usoni watakaoathirika sana na ugonjwa huu ni vijana wa Kenya hasa wanaojihusisha na tabia hatari ambazo zinachangia upataji wa saratani. Walibaini kuwa vijana wengi nchini Kenya hawana maarifa ya kutosha kuhusu saratani, namna ya kupimwa ugonjwa huo na jinsi ya kuzuia baadhi ya saratani hasa zinazohusu namna watu wanavyoishi kila siku.

Naye Ondimu na wenzake (2016) walibaini kwamba vijana wana habari finyu kuhusu umuhimu wa kwenda hospitalini ili ufanyiwe skrini ya mwili kuhusu saratani. Isitoshe, waligundua kuwa kutokana na habari finyu kuhusu saratani, kuna unyanyapaa wa hali ya juu kwa wale wanaougua ugonjwa huo. Wanaeleza kuwa katika mtaala wa elimu ya shule ya upili, hakuna taarifa ya kutosha kuhusu saratani. Wanasema sababu mojawapo ya hali hii ni kuwa waundaji mtaala wanahisi wanafunzi bado wachanga na wengi huhisi ugonjwa wa saratani huathiri wazee tu, jambo ambalo si kweli kwani saratani inawaathiri moja kwa moja au kupitia wanajamii katika mazingira wanamokulia.

Kupitia wimbo wa Steve Kay *Cancer Ina Tiba*, mwalimu anaweza kuwasaidia wanafunzi kutambua aina mbalimbali za saratani ambazo mwimbaji ametaja kama vile saratani ya matiti, kizazi,

koo na tezi kibofu. Anaeleza dalili za saratani hizo katika lugha ya kienyeji. Hapa mwalimu anaweza kuwaeleza wanafunzi wanaofahamu lugha hiyo kutafsiri hadi lugha ya Kiswahili. Kando na kufundisha suala hili la saratani, watakuwa wanajifundisha lugha ya kienyeji ambayo inasisitizwa katika Mtaala wa Umilisi. Anaimba kuwa:

> *Cervical cancer uwitsanga ava mai vari na abnormal bleeding nemwa khufula ka machi machafu.*
> Saratani ya kizazi huathiri akina mama (ila ni muhimu mwalimu awaeleze kuwa sio akina mama tu, bali wanawake wote) na hudhihirika kupitia ufujaji wa damu kwa njia isiyo kuwa ya kawaida ama kutokwa na maji machafu katika sehemu ya kizazi.
>
> *Breast cancer tsidalili tsiavwe tsivenzangu rivimba mwituru, namwa sidonda mwituru*
> Saratani ya matiti dalili zake ni kuvimba chuchu ama kidonda kwenye chuchu.
>
> *Prostate cancer ivenzangu khu ua papa onyola va papa avatsanga nende sindu vuu blocked urine nende ka makumba kachuna.*
> Saratani ya tezi kibofu huathiri akina baba (hapa pana haja ya mwalimu kusisitiza kuwa sio baba tu bali wanaume kijumla) ambapo baba anaziba sehemu ya kutoa mkojo ama anaumwa mifupa.
>
> *Throat cancer yensanga nende na khu strainer tsi sauti vaimbaji, varwaji, onyola uri nende ekhokapira ikhuchuna, uri nende nomira sindu, esauti eri inga rough.*
> Saratani ya koo huja kwa kutumia koo kwa mkazo kupindukia hasa miongoni mwa waimbaji na wahubiri. Dalili zake ni kuwa na kikohozi isiyo ya kawaida ama unapata matatizo kumeza kitu.
>
> *Then general symptoms… omundu augaha vutzwa namwe rivimba namwe sidonde sikhaona taa*.
> Alafu dalili za kijumla…mtu anakonda bure tu, ama anavimba, ama anakuwa na kidonda kisichopona.

Kando na kutaja aina na dalili za saratani mbalimbali, anaimba kuwa saratani ina tiba ikiwa itagunduliwa mapema. Mwalimu anaweza kuwaeleza wanafunzi umuhimu wa kwenda hospitalini kila mara ili wapimwe na kusisitiza kuwa waeleze wazazi wao nyumbani umuhimu huu kwani Mtaala wa Umilisi unasisitiza elimu kuwa endelevu hadi nyumbani. Isitoshe, mwalimu anaweza kuwaeleza hatua za kujiangalia matiti kwa wasichana na tezi kibofu ili kuchunguza ikiwa pana uvimbe wowote. Zaidi ya hayo, wasichana wanapaswa kushauriwa kuwa wakiona jambo lisilo la kawaida kama kutokwa kwa damu kupindukia ama maji machafu kuwatoka, basi wasinyamaze bali waeleze wakubwa wao yaani wazazi. Walimu au wahudumu wa afya ili watibiwe. Mwimbaji anaeleza kuwa watu waepuke uvutaji wa sigara. Ulaji wa mafuta mengi kwenye chakula kwani inachangia ukuaji wa saratani mwilini na kusisitiza watu wazingatie ulaji bora na kufanya mazoezi ili kudumisha siha njema na kuepuka baadhi ya saratani.

Katika wimbo huu, mwimbaji anataja baadhi ya vigogo waliougua saratani na kuaga dunia kama vile Wangari Maathai ambaye ni alikuwa mwanamazingira, Ken Okoth ambaye alikuwa mbunge nchini Kenya na Bob Collymore ambaye alikuwa mkurugenzi wa kampuni ya simu na mawasiliano Safaricom. Hali hii inaonyesha kuwa ni ugonjwa ambao unaathiri kila mwanajamii, awe tajiri au maskini, mkubwa au mdogo. Kijumla, mwalimu anaweza kutumia wimbo huu kuwaelimisha wanafunzi ambao wanaweza kuwaelimisha wanajamii wengine kuhusu saratani. Hali hii itachangia ukuaji wa jamii iliyo na maarifa na kwa wanaougua kuwa na matumaini kuwa saratani sio hukumu ya kifo na kupunguza unyanyapaa miongoni mwa wanajamii.

**Afya ya Kiakili**

Kulingana na takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani, mtu mmoja kati ya watu wanne ulimwenguni anaugua ugonjwa wa kiakili. Tafiti zimefanywa ulimwenguni na kuonyesha kuwa takribani asilimia ishirini ya wanafunzi kufikia miaka kumi na nne wameonyesha dalili za kuugua magonjwa ya kiakili. Magonjwa haya huchangia wao kuwa na tabia hasi hasa wanapobalehe. Matokeo ya utafiti wa Magai na wenzake (2018) ulionyesha kuwa asilimia kumi hadi hamsini ya watoto wadogo na waliobalehe walikuwa na matatizo ya kiakili. Matatizo ya kiakili miongoni mwa wanafunzi huchangia matokeo duni (Rothi na Leavey, 2006). Mbwayo na wenzake (2020) wanasema kuwa matatizo ya kiakili miongoni mwa wanafunzi huchangiwa na kutofanya vizuri masomoni, changamoto za nyumbani kama wazazi kuzozana, masuala ya mahusiano ya mapema na matumizi ya dawa za kulevya. Nyutu na Bertel (2012) wanaeleza kuwa walimu nchini Kenya wana jukumu muhimu sana katika kuwaelimisha wanafunzi kuhusu masuala yanayohusu afya ya akili. Hii ni kwa sababu walimu wana ukuruba wa karibu na masaa mengi na wanafunzi. Nadharia ya Utekelezaji wa Mtaala (Gross, 1971) inasema kuwa ni muhimu mwalimu kubaini yaliyomo kwenye mtaala na kutekeleza kwa kutumia mbinu inayofaa na bunifu. Kuhusiana na suala hili la afya ya kiakili, mwalimu anaweza kuwaelekeza wanafunzi wake kwa kutumia wimbo wa King Kaka unaoitwa *Beshte Yangu*. Mwimbaji anasema kuwa ni sawa kutokuwa sawa na ikiwa kuna kitu kinachokukwaza, ni muhimu kuongea usikike ili usaidiwe. Mwalimu anaweza kutumia wimbo huu kuwapa moyo wanafunzi wanaopitia changamoto na wanajihukumu kuwa wasiwe wagumu kwao kwani wao ni binadamu. Pia, anaweza kuwapa moyo kuzungumza changamoto zao na walimu wa ushauri ama yeyote aliye mkubwa wao na wanamwamini. Zaidi ya hayo, kupitia wimbo huo anaimba kuwa amemtafuta rafiki yake ambaye wanataka kuongea yanayomsuta akilini. Anasema…*uko pande gani nitokee…lets talk about it and we can always adjust the plan…*kupitia maneno haya, mwalimu anaweza kuwatia moyo wanafunzi kuwasikiliza wenzao wanaopitia changamoto za kimaisha. Kupitia wimbo wa Georgey Keith *Mental Health* inayosema kuwa kujiua si suluhisho unaposongwa na mawazo, mwalimu anaweza kuitumia kufundisha wanafunzi kuwa kujiua hakutatui jambo. Pia, mwalimu anaweza kuhakikisha kuwa mazingira ya shule ni salama kwa mtoto kusema matatizo yake bila kubaguliwa au kusemwa. Aidha, mwalimu anaweza kuwashauri wazazi kuzungumza na watoto wao na kuwasikiliza kwa njia ya upendo ili wawe na ujasiri wa kuzungumza na wao kuhusu yanayowasonga moyoni na akilini. Isitoshe, mwalimu anaweza kuwaambia wanafunzi wakachanganue wimbo wa Sauti Sol wa *Brighter days* anapowatia moyo kuwa wanapopitia changamoto za maisha, wasikate tamaa kwani ni mapito na siku bora zaja. Pia, wasife moyo kwa sababu changamoto hizo huwafanya wakawa na ujasiri wa kutatua watakayopata siku za usoni na kuwasaidia wenzao ambao wanaweza kuwa na matatizo hayo siku za usoni. Mbwayo na wenzake (2020) katika utafiti wao walipata kuwa suala la VVU/UKIMWI pia huchangia matatizo ya akili. Unapata kuna baadhi ya watoto wanaambukizwa wanapobalehe na kujihusisha na ngono za mapema. Katika wimbo wa *Beshte yangu*, mwimbaji anaimba kuwa…*beshte yangu akanicall kunishow thngs are not right...nikakam through…nikampata ameketi kwa bedside ameshika tama (*dalili ya kuonyesha kuwa rafiki yake anasongwa na mawazo kuhusu jambo fulani) …*akanishow things are not okay, the test is not good.* Mwimbaji kwa upande mwingine anamtia moyo na kumwambia inawezekana akaishi maisha marefu akizingatia maelekezo ya daktari na asifikirie kupoteza mwelekeo wa maisha yake. Mwalimu anaweza kutumia wimbo huu kuwaelimisha wanafunzi kuhusu kutoruhusu ugonjwa wa VVU/UKIMWI kuchangia kuwa na mawazo mazito ambayo yanaweza kuchangia magonjwa ya akili kwani yeyote akifuata maelekezo ya daktari ataishi.

**Suala la Uhifadhi wa Mazingira**

Mwanafilosofia Mahatma Gandhi aliwahi kusema kuwa unapaswa kuwa badiliko ambalo unataka kuliona ulimwengu. Maelezo yake yanafaa mijadala inayohusu masuala ya uhifadhi wa mazingira. Ni jukumu la kila binadamu kuchangia katika uhifadhi wa mazingira. Burton (2007) anaeleza kuwa uhifadhi wa mazingira unahusu kutunza mimea na wanyama kutokana na uharibifu au hatari yoyote. Hili ni suala mtambuko kwa sababu mazingira yasipolindwa huathiri jamii yote kwa njia hasi. Kwa mujibu wa Katiba ya Kenya (2010) sura ya tano kifungu cha pili, ni wajibu wa kila mtu kushirikiana na serikali kutunza mazingira na kuhakikisha maendeleo endelevu kiekolojia. Pia, wanyama

wanapaswa kulindwa kutokana na hatari yoyote, uwindaji haramu au kazi zozote zinazowadhulumu. Sheria nchini Kenya inasema kuwa yeyote anayepatikana akiwadhulumu, atahukumiwa kifungo cha miezi sita au faini ya shilingi elfu tatu. Pana haja ya walimu kuwafundisha wanafunzi kuhusu uhifadhi wa mazingira na haki za wanyama wawe wa nyumbani au mwituni kwani wana faida kwa jamii.

Katika kufundisha suala hili, mwalimu anaweza kutumia nyimbo kadhaa za kizazi kipya zilizo na maudhui kuhusu mazingira, ili kuwapa wanafunzi uhalisi jinsi mambo yalivyo kuhusu mazingira. Kwa mfano wimbo wa Parking Lot Grass unaoitwa *Wanyama wa Pori* unaeleza kuhusu dhuluma ambazo wanyama wa pori hasa ndovu hupitia katika mikono ya wawindaji haramu. Kuna ubeti wa wimbo wao unaosema *sielewi kwa nini tuwachinje, tuuze pembe ya nini, wanyama wa pori watabaki ni stori…*Hapa, wanahimiza umuhimu wa kuwalinda wanyama wa pori ili vizazi vya siku za usoni wapate fursa ya kuwaona porini ama kwenye mbuga za wanyama na sio tu kuwasoma vitabuni tu. Katika wimbo huu, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi kutaja aina mbalimbali za wanyama wa pori, na baadhi ya dhuluma zinazotendewa wanyama na namna ya kukabiliana na dhuluma hizo.

Wimbo mwingine ambao mwalimu anaweza kutumia kufundishia suala hili ni wimbo wa Ameru Crew *Mazingira*. Katika wimbo huu wanaeleza kuwa uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila Mkenya. Wanasema kuwa, pana haja ya serikali na jamii nzima kujukumika katika kupambana na wawindaji haramu ambao wanawaua ndovu na kuchukua pembe zao ili kuziuza katika biashara za magendo. Pia, wanaeleza kuwa pana haja ya kuhifadhi misitu kwani ukataji wa miti unaharibu makao ya wanyama na chemichemi ya mito na hivyo kusababisha wanyama kuja kwenye makao ya binadamu na ukame mtawaliwa. Katika wimbo huu, wanataja kuwa idadi ya ndovu imekuwa ikidorora nchini Kenya. Kwa mfano, mwaka wa 1970, kulikuwa na ndovu milioni moja nchini na kufikia mwaka wa 2013 walikuwa wamepungua hadi laki tano. Kupitia wimbo huu, mwalimu anaweza kujadiliana na wanafunzi kuhusu baadhi ya adhabu ambayo wawindaji haramu wanaweza kupewa na njia ya kuhakikisha misitu imehifadhiwa kikamilifu.

**Suala la Ugaidi**

Ugaidi ni suala mtambuko ambalo limeathiri nchi ya Kenya kwa njia hasi. Wakenya wengi wamepoteza maisha yao na wapendwa wao kutokana na mashambulizi ya kigaidi. Darden (2019) anaeleza kuwa kuna makundi mengi ya kigaidi ulimwenguni kama vile Al Shabab, Al Qaida, na Boko Haram. Makundi haya hutumia vijana kutekeleza shughuli zao haramu. Vijana hawa hujiunga na makundi haya haramu kutokana na ukosefu wa ajira, kijiografia unapata wapo karibu na ngome za magaidi hawa, mtazamo wao kuhusu masuala ya uchumi na hisia zao kuhusu namna walivyotengwa kisiasa na serikali. Anaeleza kuwa pana haja ya jamii kuchukua hatua za dharura katika kutatua matatizo yao na njia mojawapo anayopendekeza ni kuwashauri na kuwaongoza vijana. Vijana wanaweza kuelezwa madhara ya ugaidi kwa kutumia nyimbo za kizazi kipya ambazo wao hujihusisha nazo na hivyo kubadilisha misimamo yao. Mifano ya mashambulizi ya kigaidi nchini Kenya ambayo mwalimu anaweza kuwatajia wanafunzi ni shambulizi la Westgate, Dusit, Mpeketoni na Chuo Kikuu cha Garissa.

Mwalimu anaweza kutumia wimbo wa Ythera *Like the Phoenix, Let's All Rise,* kuwashauri wanafunzi kuhusu umuhimu wa kuwa na umoja na msimamo thabiti kama taifa ili wasikubali kuingizwa katika makundi haramu wala kuhangaishwa na magaidi hao. Mwimbaji anasema *usalama wetu ni maendeleo yetu,* kumaanisha kuwa wanafunzi wanapaswa kujua ikiwa kuna usalama nchini, basi patakuwa na utulivu na uchumi utastawi. Katika wimbo huu, mwimbaji anaeleza kuwa hata ingawa magaidi watashambulia mataifa, kuua baadhi ya wananchi na kuharibu mali, wananchi hawapaswi kuhofia. Wananchi wanapaswa kuungana, wafanye kazi kwa pamoja na wakemee vitendo hasi vya magaidi. Kutokana na maelezo hayo, mwalimu anaweza kuwashauri wanafunzi kuwa waangalifu na kuripoti mshukiwa yeyote au vitendo vinavyoshukiwa kuwa vya kigaidi katika vituo vya usalama au shuleni kwa walimu. Hili litasaidia katika kuhakikisha kuwa hatua mwafaka inachukuliwa ya kulinda taifa na wanafunzi watakuwa wanatekeleza wajibu wao wa kulinda nchi ya Kenya.

**Suala la Vita vya Kikabila na Vita vya Baada ya Uchaguzi**

Vita vya kikabila mara nyingi hushuhudiwa wakati wa uchaguzi nchini Kenya. Kulingana na makala aliyoandika Johnson (1914) anaeleza kuwa vita ni janga ambalo kila kiumbe huhusishwa na huleta hatari, machungu, kudodora kwa uchumi na vifo. Anasema kuwa hakuna mwananchi ambaye ni mzalendo atataka kuhusika vitani.

Mwisho wa mwaka wa 2007, Kenya ilishuhudia vita vikali vya baada ya uchaguzi. Kulingana na ripoti ya Kituo cha Mikakati na Mafundisho ya Kimataifa (2009), zaidi ya watu laki tatu walipoteza makazi yao, wengi walibakwa na kuuawa na mali ya kibinafsi na umma kuharibiwa katika vita hivyo. Walibaini kuwa waliopanga vita walikuwa wanasiasa na wafanyabiashara waliowatumia vijana kupigana vita hivyo. Kutokana na athari hasi za vita hivi, pana haja ya wanafunzi kufundishwa umuhimu wa amani na kuwa na msimamo imara ili wasitengwe kikabila na wanasiasa wakati wa kupiga kura. Wanapaswa kukumbushwa kuwa wao ni jamii moja na pana haja ya kuishi kwa amani.

Katika wimbo *Tuko Rada* ya Juliani, anawaeleza vijana kuwa *tusibleed ndio walead.* Mwalimu anaweza kutumia mshororo huu kuwashauri wanafunzi kuwa wasikubali kutumiwa kupigana na vijana wenzao ili viongozi wanaowatumia waweze kuongoza. Pana haja ya vijana hawa kupendana na kuishi kwa umoja kwani hakuna faida yoyote ya kumuua jirani au kijana mwenzako. Vijana wote wana jukumu la kuhakikisha kuna amani kila mwaka wa uchaguzi. Mwimbaji anawakumbusha *kama si sisi ni nani*, mshororo mwingine ambao mwalimu anaweza kutumia kuwasisitizia wanafunzi kuwa wana uwezo wa kufanya maamuzi ya busara.

Wimbo wa *Post Election Violence* ulioimbwa na kundi la vijana linaloitwa Kamata Group wanaimba:

> *Hakuna haja ya kuzozana bure, nchi yetu ni fahari yetu, hamna haja ya kuiharibu, Twamalizana sisi kwa sisi, jirani yako sio adui yako, tuwache vita tujenge Kenya…silaha tuweke chini Mungu ametubariki na nchi iliyo na uzuri na kimbilio…*

Mwalimu anaweza kutumia ubeti huu kusisitizia wanafunzi umuhimu wa amani kwani nchi ya Kenya ina mengi mazuri na hata mataifa jirani wanapozozana na kupigana, wananchi wake hukimbilia nchi ya Kenya.

Vita hivi havipiganwi tu uso kwa uso, bali vimejitokeza mitandaoni ambapo vijana hurushiana cheche za matusi kwenye majukwaa ya kijamii. Kupitia wimbo wa Sauti Sol *Tujiangalie,* wanamuziki wanaeleza kuwa kama taifa tupo pabaya kwani *tuko kwa twitter tunajibizana*. Wanaonya dhidi ya tabia hiyo ambayo inaturudisha nyuma kama taifa. Kwa hivyo, pana haja ya walimu kuwafundisha wanafunzi matumizi bora ya mitandao ili kuwapo na nchi adilifu na yenye amani.

**Suala la Uzalendo**

Kulingana na makala yaliyochapishwa na tume inayopambana na ufisadi (2010), uzalendo ni hali ya mwananchi kuionea nchi yake fahari pamoja na historia na utamaduni wa nchi husika. Uzalendo ni jukumu la kila mwananchi. Johnson (1914) anaeleza kuwa mzalendo ni mwananchi ambaye anapenda nchi yake na wananchi wenzake. Kwa mujibu wa Kibwana (2019), nchi ambayo wananchi wake ni wazalendo hustawi katika sekta zao zote za maisha na huwa na umoja. Katika Katiba ya Kenya (2010), sura ya pili kifungu cha pili, uzalendo ni maadili mojawapo ya nchi. Kwa hivyo, pana haja ya kila Mkenya, mtoto, kijana au mtu mzima kuwa mzalendo na kujivunia nchi ya Kenya.

Mwalimu anaweza kutumia wimbo *Kenya Yetu* ulioimbwa na Dela, Avril, Nyashniski na Sauti Sol kufundisha suala la uzalendo. Katika wimbo huu, wanawasifu waliopigania uhuru wa Kenya. Hapa mwalimu anaweza kuwataja baadhi ya Wakenya waliopigana na wakoloni na kuwauliza wanafunzi wataje pia. Hii itawasaidia wanafunzi kujua umuhimu wa kulinda uhuru wa nchi. Isitoshe, mwalimu anaweza kujadili na wanafunzi historia ya nchi ya Kenya katika kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni na kudumisha mjadala huo darasani. Waimbaji hawa wanataja utajiri ulio nchini Kenya kama vile wanyama wa pori ambao wanapatikana kwenye mbuga mbalimbali nchini ambao huvutia watalii, lugha zetu na rasilimali. Hapa, mwalimu anaweza kuwaongoza wanafunzi katika kutaja mbuga za wanyama nchini Kenya, aina ya wanyama wa pori na aina mbalimbali za lugha nchini Kenya. Wanasisitiza umuhimu wa kusemezana ikiwa kuna mivutano miongoni mwa wananchi, wanahimiza

wananchi kupendana na kuzingatia umoja. Hali hii inawezekana ikiwa mwananchi anapenda nchi yake, hali inayoashiria uzalendo.

Kupitia wimbo wa Eric Wainaina *Daima Mimi ni Mkenya* mwalimu anaweza kutumia kufundisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa bendera ya Kenya pamoja na maana ya rangi ambazo zimo benderani. Kulingana na Katiba ya Kenya (2010), bendera ni mojawapo ya ishara za taifa la Kenya. Mwalimu anaweza kusisitiza umuhimu wa wanajamii kuishi kwa umoja na kuepuka migawanyo ya kikabila kwani sote ni jamii moja; Wakenya. Hii inajitokeza kwenye wimbo anaposema *tuishi kwa umoja, Kaskazini hadi Kusini, kutoka ziwa hadi pwani.* Pana haja ya kuamsha ari ya uzalendo miongoni mwa wanafunzi ili kuwapo na amani na nchi ipige hatua kimaendeleo.

**Suala la Ufisadi**

Kulingana na makala iliyochapishwa na Tume ya Kupambana na Ufisadi nchini Kenya (2010), sekta ya elimu ni muhimu sana katika kuelimisha wanafunzi kuhusu ufisadi, athari za ufisadi na jinsi ya kupambana na ufisadi nchini ili kuafikia ruwaza ya 2030. Ufisadi umekuwa janga nchini Kenya na nyimbo nyingi tu zimetungwa na wasanii wa kizazi kipya kuhusu suala hili. Baadhi ya nyimbo ambazo mwalimu anaweza kutumia kufundisha suala hili ni *Sheria* ambao umeimbwa na kundi la Sarabi na *Wajinga Nyinyi* iliyoimbwa na King Kaka.

Kupitia wimbo wa *Sheria*, mwalimu anaweza kuorodhesha athari za ufisadi ambazo zimejitokeza nchini Kenya na waimbaji wametaja katika wimbo. Kwa mfano kashfa ya mahindi, tume kubuniwa kuchunguza kashfa mbalimbali bila kutoa matokeo au mapendekezo ilhali wamelipwa. Wananchi kukosa mahitaji ya msingi kama chakula, maji, huduma za msingi kama vile elimu bora kwa watoto wao ilhali ni haki yao kwani wanalipa ushuru.

Katika wimbo wa *Wajinga Nyinyi* yake King Kaka, mwalimu anaweza kuwawekea wanafunzi wasikilize na kisha waorodheshe aina zingine zaidi za ufisadi ambazo zinajitokeza katika wimbo huo. Kwa mfano viongozi kuhifadhi hela nyingi tu katika akaunti zilizo nje ya nchi kwa sababu ni pesa ambazo wamepata kwa njia haramu na viongozi kutumia ofisi na mamlaka yao vibaya. Isitoshe, viongozi wa kanisa badala ya kukashifu ufisadi unaoendelezwa na wanasiasa, wao ndio wanaoshiriki na wao kupitia kukubali pesa ambazo ni za ufisadi kama sadaka. Mwisho, viongozi akina mama kula pesa zinazopaswa kutumiwa kununulia wasichana visodo.

Mwalimu akiwaongoza wanafunzi darasani wanaweza kujadili athari za ufisadi nchini Kenya kama inavyojitokeza katika nyimbo hizi pia wanafunzi wanaweza kutoa mifano zaidi. Athari ambazo wanaweza kudondoa kutoka kwa wimbo wa *Wajinga Nyinyi* ni bei ya mafuta kupanda, ukosefu wa njia bora za usafiri hali inayochangia kuchelewa kwa mitihani ya kitaifa kufika mashuleni. Wachezaji kukosa hela za kuwakimu wanapoenda kucheza na kuwakilisha nchi ya Kenya katika mataifa mengine, viwanda vya serikali kuanguka na wakulima kutolipwa hela. Mwimbaji anaeleza kuwa ufisadi husababisha ukosefu wa ajira, migomo ya walimu na madaktari kwa sababu ya kutolipwa mishahara au kulipwa mishahara duni. Pana haja ya viongozi kuwajibika na kutekeleza wajibu wao ili kukabiliana na ufisadi.

Kando na kutaka viongozi wawajibike, kupitia wimbo wa *Sheria*, mwalimu anaweza kuwaeleza wanafunzi kuwa ni jukumu la kila Mkenya kufuata sheria, awe kiongozi au mwananchi. Waimbaji hawa wanaimba kuwa wananchi wanapaswa kuwajibika katika kupambana na ufisadi, jambo ambalo mwalimu anapaswa kuwasisitizia wanafunzi darasani. Wanasema kuwa wananchi hawapaswi kuuza kura yao kwa kukubali leso ya bure na shilingi hamsini wakati wa kampeni. Pia, wananchi wanapaswa kuacha tabia ya kutoa hongo na kutumia njia za mkato wanapotaka huduma kutoka katika ofisi za serikali au za kibinafsi.

Nyimbo hizi zinasisitiza umuhimu wa kila mwananchi kuchukua hatua ya kukomesha ufisadi. Haya ni mambo ambayo mwalimu anaweza kuwafundisha wanafunzi na hata akazua mjadala miongoni mwa wanafunzi kuhusu namna ya kukabiliana na janga hili la ufisadi.

**Suala la Ajira na Bidii**

Lengo mojawapo katika kufikia maendeleo endelevu ni kupambana na umaskini barani Afrika kufikia mwaka wa 2020. Njia mojawapo ya kutimiza lengo hili ni kuwafundisha wanafunzi njia mbalimbali za kujitegemea, kujiajiri na kuwasaidia kuondoa mawazo potofu kuhusu ubaguzi wa ajira.

Wanapaswa kutiwa moyo wafanye bidii sio tu katika kazi za shuleni, bali hata katika kazi za nyumbani.

Katika Mtaala wa Umilisi, matumizi bora ya fedha na kutia bidii ni suala ambalo ni mtambuko kwa hivyo, wanafunzi wanapaswa kufundishwa njia halali za kupata hela na matumizi bora. Kutokana na wimbo *Bidii* wake Marlow, mwanamuziki anaimba kuwa anajuta kipindi ambacho alilaza damu kwani alilala njaa. Isitoshe anajuta kutojua namna ya kutumia pesa zake vyema kwa kutokuwa na maarifa ya kuunda bajeti. Sasa anaeleza amejifunza kazi, ana biashara ndogo na hata kama hajapewa kila kitu na Mola, anasema amepewa akili, miguu, mikono ili atumie kujikimu na sasa hachagui kazi. Kupitia wimbo wa Marlow unaoitwa *Bidii*, mwalimu anaweza kuwafundisha wanafunzi umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii, kutobagua kazi, na namna ya kuunda bajeti ili wadumishe matumizi bora ya pesa.

Pana haja ya kuwahamasisha vijana wa karne hii kuhusu umuhimu wa kuwa wabunifu, kujiajiri na kutobagua wala kudharau kazi. Hili ni jambo linalosisitizwa katika Mtaala wa Umilisi. Mwalimu anaweza kutumia wimbo wa Nameless *Salari* unaoeleza kuwa kila mja anapaswa kujikaza kwa yale anayofanya. Anaorodhesha aina mbalimbali za kazi katika wimbo wake kama vile: *wenye suti mjikaze, mama mashambani, bodaboda, wenye vibarua, wamathree (matatu) na wasanii.* Anaonya watu wanaofanya kazi ofisini kuwadharau wanaofanya kazi zisizo za ofisi. Kupitia wimbo huu, mwalimu anaweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa namna ulimwengu ulivyo na kukubali uhalisi kwamba sio kazi za ofisi tu ndizo kazi bali kazi za mikono, na kujiajiri ni kazi pia. Hali hii ya wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kuhusu kazi za mikono inatokana na mtaala wa awali (8-4-4) ambao haukuchochea ubunifu miongoni mwao. Isitoshe, wasipopata ajira, wanakuwa na msongo wa mawazo na wengine hujitia kitanzi. Ni hali inayosikitisha na King Kaka ameimba kwenye wimbo wake *Wajinga Nyinyi* kuwa *system ya education in uduu, graduates wanashika placards kwa traffic, mtu wa actuarial science anataka kujimada*.

**Suala la Ngono Miongoni mwa Vijana**

Utafiti uliofanywa na Martson na wengine (2013) ulibaini kuwa barani Afrika, vijana wengi hujihusisha na masuala ya ngono kabla ya miaka ishirini. Ni miaka ambayo wengi huwa ni wanafunzi katika shule ya upili. Kutokana na hali hii, wengi wao hupata mimba za mapema, wengine hujaribu kuavya na matokeo huwa kifo kwa mtoto anayeavya na anayejaribu kumuavya. Pia, ngono za mapema miongoni mwa vijana huchangia maambukizi ya magonjwa ya zinaa na wengine huishia kuacha shule. Watafiti hao wanapendekeza kuwa pana haja ya vijana kushauriwa kuhusu masuala ya ngono na umuhimu wa kuchukua tahadhari ya kulinda maisha yao.

Mwalimu katika Mtaala wa Umilisi ana jukumu muhimu la kuwashauri wanafunzi au vijana kwa sababu ana ukuruba na hutangamana na wanafunzi kwa muda mrefu. Mwalimu anaweza kutumia wimbo wa Sauti Sol *Take It Slow* anapowashauri kuhusu suala hili. Katika wimbo huu waimbaji wanaimba:

> *…najua kweli unataka, pia mimi nataka, But niko na baba ndani ya maisha so inabidi niombe nipate self control kesho tusipatane na ma control. Hii mambo ni ngori maisha si movie usije kesho ukasema weeeh!*

Katika wimbo huu, mwalimu anaweza kuwashauri kuwa licha ya haja za kibinadamu za kutaka kujihusisha na ngono, mja ana uwezo kudhibiti hali hiyo ili asije akajuta. Anaweza kujidhibiti kwa kujihusisha na masuala mbalimbali kama kusoma, kufanya mazoezi na kuhakikisha hajipati katika hali ambazo zinaweza kuchochea au kumtia majaribuni. Ni muhimu wanafunzi kushauriwa kuishi maisha yao na kutosheka na yale waliyo nayo. Pia, ni muhimu waambiwe kuwa wasiwe na pupa kwani katika maisha ya sasa ambapo vigezo vya maisha bora ni namna wasanii na watu maarifa wanavyoweka picha mitandaoni, wakati mwingine hali halisi sio hiyo. Katika wimbo huu, wasanii wanasema kuwa *kimo cha maisha ni Instagram, tukibishana na swag, mali ya kuazimwa ikiwaka…*wanapaswa kushauriwa kuwa wasilinganishe maisha yao na yale wanaoyaona mtandaoni. Hii itawasaidia kuepukana na msongo wa mawazo wa kutaka kuishi maisha ambayo hawayawezi

kwani wengi wameparamia maisha hayo kwa pupa na kupotoka kabisa na hata kufa kutokana na tamaa.

**Hitimisho**

Pana haja ya kuwafundisha wanafunzi masuala mtambuko kupitia njia bunifu ili wawe na uwezo na ujasiri wa kukabiliana na masuala haya katika mazingira wanamokulia na hivyo kuwa na jamii inayokaribia kukamilika katika masuala ya uchumi, siasa na jamii. Katika Mtaala wa Umilisi ambapo mwanafunzi anapashwa kushirikishwa katika zoezi zima la ujifunzaji, nyimbo za kizazi kipya ni njia mojawapo inayoweza kutumika. Njia hii ni madhubuti kwani kwanza watoto au vijana hufurahia sana nyimbo. Kwa kutumia nyimbo za kizazi kipya, zoezi la ujifunzaji darasani huweza kurahisishwa zaidi. Ili kufanikisha sasa ujifunzaji huu wa masuala mtambuko, mwaimu hana budi kufahamu mtaala husika na kutumia mbinu ya nyimbo za kizazi kipya kutekeleza ufundishaji wa masuala haya.

**Marejeleo**


Abuya, B. (April, 3 2017). Why the new curriculum is a triumph for Kenya's children. *The Conversation.*

Busolo, D., Woodgate, R.L., na Decker, K. (2018). Kenyan youth understanding of cancer, cancer risk and cancer prevention: An ethnographic study. Katika *Journal of Global Oncology.* Vol 4 (2).

Centre for Strategic and International Studies (2009, August). Post election violence in Kenya and its aftermath.

Darden, J.T. (2019). *Tackling terrorists' exploiting of youth*. America Enterprise Institute.

Gitau, A.W., Wanyama, E. W. na Kevogo, S. A. (2023). Tathmini Mbinu za Ufundishaji wa Masuala Mtambuko katika Mtaala wa Umilisi: Mfano wa Shule za Msingi za Nchini Kenya. Katika *East African Journal of Swahili Studies, 6(2). Kur.73-83*

Government of Kenya. (2010). *The Constitution of Kenya*. Nairobi: The Government Printer.

Gross, N. (1971). *Implementing Organizational Innovation. A Sociological Analysis of Planned Educational Changes.* Newyork: Basis Book Inc.

IBE-UNESCO (2017). "The why, what and how to competency based curriculum reforms: The Kenyan experience." Katika *Progress Reflection NO. 11 on Current and Critical Issues in Curriculum Learning Assessment*.

Johnson, S. (1913). The patriot. Katika *The Works of Samuel Johnson*. New York: Pafraet and Co Troy.

K.I.C.D. (2017). *Basic education curriculum framework: Nurturing every learner's potential.* Nairobi: Kenya Institute of Curriculum Development.

Kebaya, C. na Wanjala, H. (2016). Popular music and identity formation among Kenyan youth. Katika *Muziki.* Juz.13(2). Kur. 20-35.

Kenya HIV Estimates. Report 2018. Ministry of health. Maidha national AIDS control council. Nationa AIDS and STI Control program.

Kenya my country: Rekindling the spirit of patriotism. (2010). A publication of Ethics and Anti Corruption Commission: Education Department.

Khalili, E. (2018). "Uimarishwaji wa Umaizi Mseto kupitia Mikakati Shirikishi ya Ufundishaji wa Kiswahili nchini Kenya." Katika *Proceeding of the 1st Annual International Conference held on 17th-19th April 2018.* Chuo Kikuu cha Machakos, Kenya.

Kibwana, K. (2019). Patriotism is a national duty: Lets promote it. *Daily Nation,* Nairobi: Nation Media Group.

Koster, M. M. (2013). The hiphop revolution in Kenya: Ukoo Flani MauMau, Youth, politics and memory 1990-2012. Katika *The Journal of Pan African Studies*. Juz. 6 (3).

Martson, M., Beguy, D., Kabiro C. na Cleland, J. (2013). Predictors of sexual debut among young adolescents in Nairobi informal settlements. Katika *International Perspectives on Sexual and Reproduction Health*. Vol.39 (1).

Magai, D. N. Malik, J. A na Koot, H. M. (2018). Emotional and behavioural problems in children and adolescents in Central Kenya. Katika *Child psychiatry and human development. Vol.49(4). Uk. 659-671*

Mbwayo, A.W., Mathai, M., Khasakala, L.I. Kuria, M.W, na Stoep, A.V. (2020). Mental health in Kenyan schools: Teachers perspective. Katika *Glob Soc Welf.* Vol.7. Uk. 155-163

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi ya Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mwangi, E. (2004). 'Masculinity and nationalism in East African hiphop music' katika *Tydskrifletterkunde,* 41 (2) uk. 5-20.

Mwangi, E. (2009) Violence, sex and hiphop hype. *Sunday Nation,* Nairobi: Nation Media Group.

NACADA. (2016, October). National survey on alcohol and drug abuse among secondary school students in Kenya. Survey report.

Njogu, K. (2009). It is unacceptable to determine boundaries of intellectual work. *Sunday Nation*, Nairobi: Nation Media Group.

Ntarangwi, M. (2009). *East African hiphop*: Youth, culture and globalization. University of Illinois Press.

Nyutu, P.N. na Bertel, J.M. (2012). Perceptions of teacher preparation and attitudes regarding students' mental health in Kenya. Katika *Advances in schools' mental promotion*, 5(1). Uk.63-74

Omollo, G.O., Odongo, B.C. na Raburu, P. (2016). School based factors affecting the teaching of Kiswahili in public pre school in Kasipul divison, Rachuonyo South sub county. Katika *International Journal of Education and Research.* Vol.4. No.3. Uk.323-350.

Ondimu, S.M. (2018) Teachers preparedness for the implementation of Competence Based Curriculum in private pre schools in Dagoretti sub county Nairobi city County. Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi.

Ondimu, T.O., Amimo, F.A., Odado, P.S. na Sereta, B. (2016). Factors that influence the uptake of breast cancer screening among secobdary school students: A case of Kisii South Sub Count. Katika *Oncology Case Rep.* Juz.1 (109).

Owala, O.R. (2021). Success and challenges of implemtation of Competence Based Curriculum in Kenya.

Perullo, A. (2011). Politics and popular songs: Youth, authority and popular music in East Africa. Katika *Africa Music.* Juz. 9 (1). Uk. 87-115.

Rothi, D.M. na Leavey, G. (2006). Mental health help seeking and young people: A review, Katika *Pastoral care in education*. Vol. 24(3) Uk.4-13.

Sifuna, D.N. na Obonyo, M.M. (2019). Competence Based Curriculum in primary schools in Kenya: Prospect and challenges pf implementation. Katika *Journal of popular education in Africa.* 3(7). Uk. 39-50.

Sultana, N. na Naseem, M. (2012). Contemporary issues and trends in education. Katika *Window on practice guide*.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Kenya: Oxford University Press.

Wasike, M. W. (2015). Tathmini ya matumzi ya nyimbo za kizazi kipya kama mbinu ya kufundishia masuala ibuka katika Kiswahili kwenye shule za upili nchini Kenya. Kibabii University. Bungoma: Kibabii University.